

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa ya kuajiriwa kwa muda mfupi katika Kitengo cha Uchapaji na Uchapishaji katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) kama ifuatavyo:

Jina la kazi: Msaidizi wa Ofisi (Nafasi 7)

A: Sifa na Uzoefu Unaohitajika

- i. Awe raia wa Tanzania.
- ii. Awe na umri usiozidi miaka 40 wakati analeta maombi.
- iii. Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- iv. Awe na ujuzi wa masuala ya uchapaji na uchapishaji.
- v. Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili katika masuala ya uchapaji na uchapishaji.
- vi. Awe na ujuzi wa aina na vipimo vya karatasi.
- vii. Awe ni mwenye kujituma na kufanya kazi katika timu.
- viii. Ujuzi wa kompyuta, uhariri, kusanifu majarada na kuseti miswada ni sifa muhimu ya ziada.

B: Wajibu na Majukumu

- i. Kuendesha mashine za uchapaji.
- ii. Kukata, kukunja, kuchanganya na kukagua karatasi za machapisho.
- iii. Kukagua na kubaini machapisho 'perfect bind' na 'saddle stich'.
- iv. Kupesti miswada.
- v. Kugonga namba machapisho.
- vi. Kupiga pini vitabu na machapisho mengine.
- vii. Kupanga, kupakia na kuhesabu vitabu.

C: Nyaraka Muhimu za Kutuma:

- i. Barua ya maombi.
 - ii. Wasifu binafsi.
 - iii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha uraia.
 - iv. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne.
-

Maombi yatumwe kwa baruapepe: iks@udsm.ac.tz

**Mkurugenzi
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
S.L.P. 35110
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/12/2022